




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA KIGOMA



Tel. 028 280 4865  
Fax No. 028 280 2370  
Email: ded@kigomadc.go.tz

Kumb.Na KDC/D3/242/115



Ofisi Ya Mkurugenzi Mtendaji,  
S.L.P. 332,  
KIGOMA.

Tarehe 02/10/2024

**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA  
WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAMU  
(Limetolewa kwa kuzingatia kanuni ya 7{1})**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya Kuvikopesha vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu, ambapo jumla ya shilingi **200,380,614/=** zimetengwa katika robo ya 2 ya Mwaka wa fedha 2024/2025. Hivyo, vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kupeleka maombi kwenye ofisi za Vijiji au Kata zilizopo katika Maeneo yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

- kikundi cha Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu kiwe kimetambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na halmashauri
- Kikundi kiwe kinachojishughulisha na Ujasiriamali mdogo, wa kati au mkubwa au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za Ujasiriamali
- Kikundi cha Wanawake na Vijana kiwe na idadi ya Wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na Watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili(2), pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a(1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo timu ya menejimenti ya halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana nae katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine.
- Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kijasiriamali, na
- Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania, Wawe na NIDA, wasio na ajira rasmi au wananufaika na pesheni, wenye akili timamu, na wenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha Vijana kinapaswa kuwa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroniki (tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa kata au Afisa Mtendaji wa kata husika


Kikundi kinachooomba Mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo:-

- Barua ya Maombi ya Mkopo ilipitishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji

- Muhtasari wa Kikundi wa kuomba mkopo na uwe na Mahudhurio ya wanakikundi yaliyosainiwa.
- Andiko rahisi la Mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo na
- Taarifa ya akaunti ya benki au suluhisho la kibenki la hivi karibuni (Current Bank statement)

Mwisho wa kuwasilisha maombi ya mkopo ni tarehe **31** mwezi **10** mwaka **2024**.

Tangazo hili limetolewa na,



Jabil.Z. Timbako

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA KIGOMA**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
KIGOMA**